

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA**

**10 MEI, 2018**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA – TAREHE 10 MEI, 2018

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na

Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

### **III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

### **IV. MASWALI YA KAWAIDA:**

#### **WIZARA YA NISHATI:**

#### **217. MHESHIMIWA ZAINAB MNDOLWA AMIRI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Je, ni lini Serikali itapunguza bei ya gesi kwa matumizi ya nyumbani ili kuwawezesha Wananchi wengi zaidi kutumia gesi kwa matumizi yao ya nyumbani na kuondokana na matumizi ya kuni na mkaa.

#### **WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

#### **218. MHESHIMIWA DKT. SHUKURU JUMANNE KAWAMBWA (BAGAMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Upanuzi wa barabara kutoka mita 22.5 hadi 30 kutoka katikati ya barabara umesababisha baadhi ya Wananchi

katika Kitongoji cha Sanzale Kata ya Magomeni kufuatwa na barabara na nyumba zao kuwekwa X:-

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia Wananchi hao.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**219. MHESHIMIWA SUSAN LIMBWEKI KIWANGA (MLIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Jimbo la Mlimba lina mito mingi inayotiririka mwaka mzima ambayo inaweza kutumika kujenga malambo kwa ajili ya mifugo:-

Je, ni lini Serikali itajenga malambo kwa ajili ya kunyweshea mifugo katika Jimbo la Mlimba.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**220. MHESHIMIWA SHABANI OMAR SHEKILINDI (LUSHOTO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Wilaya ya Lushoto haina Chuo cha Ufundi (VETA) na kuna vijana wengi waliohitimu Elimu ya Msingi na Sekondari:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga Chuo cha Ufundi (VETA) ili vijana hao waweze kupata elimu ya ufundi ya kuwasaidia katika kujiajiri.

**WIZARA YA KILIMO:**

**221. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA  
BILAKWATE (KYERWA):**

Atamuuliza Waziri wa Kilimo:- Serikali imezuia biashara ya BUTURA na wanunuzi wa Kahawa kwa watu binafsi (moja kwa moja kwa Wakulima) na kuagiza Kahawa yote iuzwe kwa Vyama vya Msingi wakati Vyama kama KDCU vilishindwa kuwapa bei nzuri wakulima:-

- (a) Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha inakuja na mbinu mpya ya kuwapatia bei nzuri Wakulima wa Kahawa;
- (b) Je, ni hatua zipi zimechukuliwa haraka ili kuhakikisha wale walioua Vyama vya Ushirika wanashitakiwa.

**V. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**DODOMA  
10 MEI, 2018**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**

